

WATORO : TUMECHOKA

MWAAFRIKA
26/6/63

SASA BAKI VITA TU

UJUMBE wa chama cha African National Congress ya Afrika ya Kusini utakapokutana na Komiti ya Uhuru wa Afrika; utajambua jinsi wananchi wa Afrika ya Kusini walivyochoshwa na mateso ya Serikali ya Makaburu na sasa wanataka msaada wa vifaa vya vita ili wazishambulie na kupindua Serikali hiyo ya Makaburu.

Ripota wetu Dar

Msemaji wa chama hicho ambacho kina makao yake makuu hapa Dar es Salaam, alisema hayo leo, (Jumanne) kwa waandishi wa Habari kabla ya kukutana na Komiti hiyo ambayo imeanza leo kufanya mkutano wake wa kwanza katika mji wa Dar es Salaam.

Komiti hiyo ambayo imehaguliwa kutoka nchi tisa za Kiafrika iliundwa mapema mwezi jana huko Addis Ababa kulikokuwa kunafanyika mkutano wa Umoja wa Afrika. Shabaha zake ni kutafuta njia zitakazowawezesha kupata uhuru wao wananchi wa Afrika ya Kusini, Angola, Msumbiji na zinginezo zingalizo bado zatawaliwa.

Nchi za Uingereza, Ufaransa na Ubelgiji zimelaumiwa na msemaji huyo kwamba zinawasaidia Makaburu katika kuwaua wananchi wa Afrika ya Kusini kwa kuwauzia ndege za kivita na nchi hizo zimeshairiwa kutafuta njia zingine za kupatia pesa badala ya kuuzia Serikali ya Afrika ya Kusini

ndege zao.

Mwisho tamko lililotolewa ni kwamba leo (Jumatano) itakuwa ni siku ya kilio cha makumbusho ya Waafrika 19 walio-uawa na polisi wa Makaburu katika mji wa Transval mnamo mwaka wa 1952 baada ya kufanya maandamano ya

kudai haki zao.

Siku ya leo itasheherekewa katika nchi zote za Kiafrika na kutafanyika mkutano wa hadhara hapa Dar es Salaam utakaohutubiwa na viongozi wa TANU pamoja na wajumbe wa Komiti ya Uhuru wa Afrika.